KENYA PRIMARY SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT

DECEMBER ASSIGNMENT 2026

GREDI YA 6 – KISWAHILI LUGHA

Muda: Saa 2

STEPPING TO JUNIOR SCHOOL

MAELEZO YA MWANAFUNZI

Jina: _____ **Shule:** _____

Nambari ya Tathmini/UPI: _____ **Tarehe:** _____

MAAGIZO KWA MWANAFUNZI

1. Andika jina lako, nambari ya Tathmini/UPI na tarehe katika nafasi ulizopewa.
2. Hakikisha kuwa karatasi hii ina kurasa zote na hakuna swali lililokosekana.
3. Soma kila swali kwa makini kabla ya kuchagua jibu.
4. Jibu **maswali yote**.
5. Chagua jibu lililo sahihi zaidi kati ya A, B, C na D.

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.

Mbweha na Fisi ni viongozi wa mataifa yao. Fisi amekuwa akikabiliwa na mzozo wa uongozi katika taifa lake. Kwa hiyo, aliamua kumtembelea kiongozi mwenzake, Bwana Mbweha, ili kupata ushauri.

Mbweha: Karibu, Mheshimiwa Rais mwenzangu.

Fisi: Asante sana, ndugu yangu.

Mbweha: Masalkheri, ndugu. Habari za kwako?

Fisi: Bado hali ni mbaya. Mambo hayajatulia. Ndiyo maana nimekuja kwako ili unishauri.

Mbweha: Ni wazi kuwa vurugu hazitakoma hadi utekeleze tuliyoshauriana kwa simu. Kumbuka kuwa vijana wa kizazi hiki hawatikisiki.

Fisi: Vijana hawa wanaojiita *Gen Z* wanataka niondoke mamlakani. Hilo siwezi kulikubali kamwe. Wananilaumu kuwa nimeongeza ushuru na ninaendesha taifa kana kwamba ni kampuni yangu binafsi.

Mbweha: Hebu nieleze, msimamo wa jeshi lako ukoje?

Fisi: Idadi kubwa ya wanajeshi wananiunga mkono. Nimezungumza na wakuu wa vikosi mbalimbali na hawataki niondoke madarakani.